

KKKT DAYOSISI YA KASKAZINI

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

KKKT Dayosisi ya Kaskazini inatangaza nafasi ya Kazi.

NAFASI YA KAZI: KATIBU IDARA YA ELIMU - DAYOSISI

SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe na Elimu ya Shahada ya Uzamili katika taaluma ya Elimu au usimamizi wa Elimu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
2. Awe na Uzoefu usiopungua miaka 10 katika usimamizi wa taasisi za Elimu
3. Awe na uelewa wa kina katika mambo yahasuyo sera, miongozo na kanuni za utoaji elimu katika nchi yetu.
4. Awe Mkristo, mwenye sifa njema ya uaminifu na anayetenda kazi kwa bidii bila kusimamiwa.
5. Awe mbunifu, mwenye uwezo wa kuandika miradi yenye lengo la kuinua ubora wa elimu katika shule/taasisi zinazomilikiwa na Dayosisi
6. Uwezo wa kufikiri kimkakati (Strategic Thinking) na kufanya maamuzi sahihi katika utoaji wa huduma za elimu kwenye mazingira yenye ushindani
7. Mwenye uwezo mzuri wa kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza
8. Awe na umri kati ya miaka 35 hadi 50

MAJUKUMU YA MSINGI

- Kuratibu na kusimamia mipango ya utekelezaji wa sera ya elimu ya KKKT Dayosisi ya Kaskazini
- Kuratibu na kutafsiri sera, kanuni na miongozo ya elimu ya Dayosisi
- Kuandaa taarifa ya mwenendo wa utoaji wa huduma za elimu katika Dayosisi utakaowasilishwa katika vikao vya Halmashauri ya Elimu na hatimaye Halmashauri Kuu ya Dayosisi
- Atakuwa mjumbe wa Bodi za shule zinazomilikiwa na Dayosisi akimwakilisha Katibu Mkuu wa Dayosisi
- Atakuwa mwandishi wa vikao vya Halmashauri ya Elimu ya Dayosisi

- Atahudhuria mikutano yote ya wadau/wasimamizi inayohusu utoaji wa huduma zaElimu/mafunzo kama vile CSSC, Uthibiti ubora nk

MUDA WA AJIRA

Ajira ni Mkataba kwa kila Miaka Mitatu [3].

MSHAHARA

Utazingatia muundo wa viwango vya mshahara kama miongozo ya KKKT Dayosisi ya Kaskazini inavyoainisha.

NJIA YA KUTUMA MAOMBI YA KAZI

Barua ya Maombi, Vyeti vya Kitaaluma vilivyothibitishwa, Barua ya Utambulisho toka kwa Kiongozi wa Dini, na picha mbili ndogo [Pasport size] za muombaji pamoja na wasifu binasi (CV) vitumwe kwa Katibu Mkuu, KKKT Dayosisi ya Kaskazini, S. L. P 195, Moshi, Tanzania.

TAREHE YA MWISHO

Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha maombi ni **03.03.2023**.

LIMETOLEWA NA,

Katibu Mkuu KKKT Dayosisi ya Kaskazini.